



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
T A WALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na +255 26 2965824  
Fax Na 255 26 2965824  
ded@urambodc.go.tz  
tovuti: www.urambodc.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji(W)  
S.L.P 170,  
URAMBO,  
TABORA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. UDC/W.1/455/112

Tarehe:18/10/2021

### TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kuwa ofisi imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu **UTUMISHI** chenye Kumb.Na. FA.170/365/01 "B"/147 cha tarehe 15 Septemba, 2021 kwaajili ya kujaza nafasi ya kazi ya **Mtendaji wa Kijiji III** kwa masharti ya kudumu. Hivyo watanzania wote wenye sifa mnakaribishwa kuomba nafasi hiyo. Maelezo ya nafasi yapo kama ifuatavyo;

#### **MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III)-Nafasi 1**

##### **i. Sifa za Kitaaluma kwa waombaji**

Kuajiriwa waombaji wenye elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) waliojipatia mafunzo katika ngazi ya Cheti (NTA Level 5) ambao wamehitimu mafunzo ya astashahada/ cheti katika moja ya fani zifuatazo;

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### **ii. Majukumu ya Kufanya**

a. Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji



- b. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa utawala Bora katika Kijiji
  - c. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
  - d. Katibu wa mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
  - e. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu
  - f. Kuaandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali
  - g. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
  - h. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
  - i. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji
  - j. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
  - k. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji
  - l. Kuwajibuka kwa Mtendaji wa Kata.
- iii. **Masharti ya Ajira:** Ajira ya Kudumu
- iv. **Mshahara:** Ngazi ya Mshahara wa kuanzia ni TGS B

### **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania
- ii. Waombaji wote wawe na umri wa kuanzia miaka kumi na nane (18) na wasiozidi umri wa miaka arobaini na tano (45).
- iii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) wenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba zao za simu.
- iv. Waombaji wote wanatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- v. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma (Certificates), Nakala ya vyeti vya kidato cha Nne (IV) au sita (VI) kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi ya mtendaji wa Kijiji na picha (Passport size) mbili za hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma. Viambatisho hivyo vibanwe pamoja kuondoa uwezekano wa kupotea. **Transcript, testimonials, provisional results, statement of results na hati za matokeo ya kidato cha Nne au Sita havitaruhusiwa.**




- vii. Kuwasilisha vyeti vya kugushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria
- viii. Waombaji ambao ni watumishi wa umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- ix. Waombaji ambao walistaafu kazi kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hii.
- x. Waombaji wote waandike namba zao za simu kwenye maombi yao kwaajili ya mawasiliano
- xi. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu
- xii. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha Nne/Sita na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE)
- xiii. Barua za maombi iandikwe kwa kiswahili/Kiingereza
- xiv. Watakoachaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya **USAILI**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 01/11/2021**

**Maombi yote yatumwe kwa;  
MKURUGEZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 170,  
URAMBO**

**Tangazo hili limetolewa na;**



**BARAKA M ZIKATIMU  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
URAMBO**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
URAMBO**